**TANGAZO LA SERIKALI NA. …….. LA TAREHE …………**

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA SURA 290**

**SHERIA NDOGO**

***(Zimetengenezwa Chini ya Kifungu 7(1) na 16(1)***

**SHERIA NDOGO YA (ADA ZA VIBALI VYA BURUDANI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA YA MWAKA, 2025.**

| | | |
|---|---|---|
| | **SEHEMU YA KWANZA** | |
| Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika | **1.** | Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya (Ada za vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ya Mwaka, 2025 na itaanza kutumika mara itakapotangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | **2.** | Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. |
| Tafsiri | **3.** | 1) Katika Sheria ndogo hii isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:<br><br>***"Ada"*** maana yake ni kiasi cha fedha kitakachotozwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa ajili ya kibali cha shughuli ya Burudani, itakayofanyika katika eneo la Halmashauri.<br><br>***"Eneo la burudani"*** ni mahali popote ambapo shughuli ya burudani inafanyika.<br><br>***"Halmashauri"*** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.<br><br>***"Kibali cha burudani"*** Maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za burudani ambayo inakutanisha zaidi ya watu kumi katika ukumbi, uwanja wa michezo au sehemu yoyote ya wazi au Mitaani.<br><br>***"Mkurugenzi"*** maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa au Afisa yeyote wa Halmashauri ya Wilaya anayekaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwa wakati huo.<br><br>***"Muda"*** Maana yake ni wakati ambao unaruhusiwa shughuli ya burudani kufanyika.<br><br>***"Shughuli ya burudani"*** maana yake ni sherehe, shughuli yoyote |

RASMI

| | | |
|---|---|---|
| | | ile ya kijamii, Sanaa na Utamaduni.<br><br>***"Afisa mwidhiniwa"*** maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii ikiwa ni pamoja na Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji. |
| | **SEHEMU YA PILI<br>UTOZAJI WA VIBALI** | |
| Wajibu wa kuwa na Kibali | 4. | 1) Hakuna shughuli yoyote ya burudani itakayofanyika katika eneo la Halmashauri bila kuwa na kibali cha maandishi kitakachotolewa na Halmashauri.<br>2) Maombi yote ya vibali yatalipiwa ada kama ilivyooneshwa katika jedwali la pili la sheria ndogo hii. |
| Utaratibu wa kuomba kibali | **5.** | 1) Mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli ya burudani katika eneo la Halmashauri atatuma maombi ya kibali kwa Mkurugenzi kupitia kwa Afisa Mwidhiniwa kwa kujaza fomu maalum kama ilivyooneshwa katika jedwali la kwanza la sheria ndogo hii.<br>2) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yataeleza jina la mwombaji, aina ya burudani, tarehe, muda wa kuanza na kumalizika kwa burudani na eneo husika.<br>3) Iwapo maombi ya kibali yatakataliwa Halmashauri itamuarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa kutoa kibali hicho.<br>4) Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatanisho vyote muhimu. |
| Wajibu wa mmiliki wa ukumbi na Nyumba za Ibada | 6. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa ukumbi wa muziki na nyumba za ibada kupiga muziki kwa kiwango cha sauti cha kawaida bila kuathiri watu wanaozunguka eneo la ukumbi huo wa mziki au nyumba ya ibada.<br>2) Kila mwonesha video au sinema atatakiwa kuweka sauti ya chini wakati wa onesho bila kuathiri majirani wanaomzunguka.<br>3) Ni wajibu wa kila mmiliki wa kumbi za burudani au baa au muziki kuhakikisha kuwa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane (18) haingii katika kumbi hizo na endapo itabainika kuingia kwa watoto hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa kumbi hizo. |
| Vigezo vya utoaji wa vibali | **7.** | 1) Halmashauri itatoa kibali iwapo itajiridhisha na mambo yafuatayo:-<br><br>(a) Shughuli ya burudani inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani.<br>(b) Eneo linaloombewa kibali cha kufanyia shughuli ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | burudani/ibada linaruhusiwa kwa shughuli inayoombewa kibali.<br>(c) Kumbi za burudani zina usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo madirisha ya kutosha ya kuingiza na kutolea hewa, milango ya dharura, umeme, milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura.<br>(d) Muda wa burudani utakuwa ni kuanzia saa 12:00 Asubuhi hadi hadi 6.00 usiku.<br>(e) Disko litaruhusiwa kupigwa siku ya ijumaa hadi jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa tatu usiku hadi saa sita usiku isipokuwa maeneo ya huduma za jamii. |
| Marufuku | 8. | 1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18 kuruhusiwa kuingia kwenye sehemu za starehe mara baada ya muda ulioruhusiwa kwisha au kulingana na Sheria ya Mtoto Sura ya 13.<br>2) Ni marufuku kwa mwenye ukumbi wa video na sinema au sehemu yeyote kuonyesha picha za video ambao hazina maadili.<br>3) Muda wa kuonyesha video au sinema utaanzia saa 8:00 Mchana hadi saa 6:00 usiku kwa siku za kazi, kwa siku za Jumamosi na Jumapili na siku za sikukuu utaanza saa 6:00 mchana hadi saa 6:00 usiku. |
| Mamlaka ya Halmashauri | 9. | 1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia mahali popote panapofanyika shughuli ya burudani au anapoamini kuna shughuli ya burudani inafanyika muda wowote kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafuata masharti ya kibali.<br>2) Katika kutekeleza mamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli ya burudani kulingana na hali itakayobainika baada ya ukaguzi kufanyika. |
| Mkusanyiko wa watoto | 10. | 1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukusanya watoto kwa ajili ya tamasha ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi cha Halmashauri.<br>2) Mkusanyiko wowote wa watoto uliopata kibali cha Halmashauri kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) utamalizika kabla ya saa 12:00 jioni.<br>3) Mtu yeyote aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atawajibika kwa usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko huo na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko.<br>4) Itakuwa ni makosa kwa mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye mamlaka juu ya mtoto kuruhusu au kusababisha kwa uzembe mtoto kuhudhuria mkusanyiko usio na kibali cha |

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| | | Halmashauri. |
| Vibali visivyotozwa Ada | 11. | 1) Mikusanyiko ifuatayo itaombewa vibali bila kulipa ada<br>a) Mikusanyo ya kidini<br>b) Misiba<br>c) Michezo ya watoto isiyotozwa |
| Usafi wa mazingira | 12. | 1) Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za burudani ndani ya mamlaka ya Halmashauri atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya burudani kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli ya burudani.<br><br>2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1) atalipa gharama ya uchafuzi wa mazingira kadri zitakavyokadiriwa na Halmashauri na gharama zingine ambazo Halmashauri itaingia katika kuondoa uchafu huo. |
| Muziki unaoleta kero | 13. | 1) Mtu yeyote aliyepata leseni ya biashara haruhusiwi kupiga muziki unaoleta kero kwa majirani na jamii kwa ujumla kwenye eneo lake la biashara.<br>2) Kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hii kitatumika sawa kwa mtu atakayekiuka kifungu kidogo cha (1). |
| Ukamataji wa vifaa | 14. | 1) Bila kuathiri ujumla wa kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hii, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vifaa vyovyote vitakavyokutwa katika shughuli ya burudani ambayo haina kibali au inaendeshwa bila kufuata masharti ya kibali.<br>2) Vifaa vitakavyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) vitachukuliwa na kuhifadhiwa katika ofisi za Halmashauri au eneo lolote litakaloamuliwa na Halmashauri.<br>3) Vifaa vilivyokamatwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi vitatakiwa kukombolewa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kukamatwa na baada ya hapo Halmashauri inaweza kuuza vifaa hivyo kwa mnada baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama.<br>4) Mtu yeyote anayetaka kukomboa vifaa vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hizi atawajibika kulipa gharama za ukamataji, usafirishaji na ulinzi. |
| **SEHEMU YA TATU**<br>**MAKOSA NA ADHABU** | | |
| Makosa na adhabu | 15. | 1) Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote kwa pamoja yaani faini |

RASMI

| | | |
|---|---|---|
| | | na kifungo. |
| Kufifilisha kosa | 16. | 1) Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) hadi shilingi laki mbili (200,000) mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum itakayotolewa na Halmashauri kama ilivyo katika jedwali la tatu la Sheria Ndogo hii. |

RASIMU

**JEDWALI LA KWANZA**
***(Imetengezwa Chini ya kifungu cha 5(1)***

**<u>FOMU YA MAOMBI YA KIBALI</u>**

(Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la mwombaji<br>................................................................. | 2. Anwani ya mwombaji<br>........................................ |
| 3. Aina ya shughuli<br>................................................................. | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli<br>........................................... |
| 5. Muda wa kuanza<br>................................................................. | 6. Muda wa kumaliza<br>.......................................... |
| 7. Ada ya kibali (TZS)<br>.............................................. | 8. Namba ya Stakabadhi ya malipo<br>........................................ |
| 9. Saini<br>………………………………… | 10. Tarehe<br>…………………….... |

**SEHEMU YA PILI (Kwa Matumizi ya Ofisi tu)**

| | |
|---|---|
| 1. Maombi<br>.............................................. | 2.Ada ya kibali Tshs<br>.......................................................... |
| 3. Namba ya stakabadhi ya malipo<br>............................................................. | 4.Tarehe ya malipo<br>........................................................... |
| 5. Jina la Afisa aliyepokea malipo<br>................................. | 5.Saini<br>..................................... |

7.Muhuri......................

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*futa isiyohusika*)Sababu:

……………………………..………………………………………………………....
Jina:…………………………………………….Saini: ……………………..……...
Tarehe:…..………..Mwezi.........................Mwaka..........................................

RASIMU

**JEDWALI LA PILI**

**( *Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(2)* **

**ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA BURUDANI, UTAMADUNI NA SANAA**

| **Na.** | **Maelezo** | **Kiwango** |
|---|---|---|
| 1. | Muziki wa Dansi | Sh. 20,000/= kwa siku |
| 2. | Muziki wa Disco | Sh. 20,000/= kwa siku |
| 3. | Shindano la kutafuta msanii | Sh. 20,000/= kwa shindano |
| 4. | Shindano la kutafuta warembo | Sh. 20,000/= kwa shindano |
| 5. | Maonesho ya mavazi | Sh. 20,000/= kwa onesho |
| 6. | Maombi ya kibali cha sherehe za unyago na ngoma na sherehe za kidini | Sh. 20,000/= kwa sherehe |
| 7. | Maombi ya kibali cha sherehe za harusi, Sendoff, kipaimara | 30,000 kwa sherehe |
| 8. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei (promotion) | Sh. 50,000/= kwa tangazo |
| 9. | Matamasha ya kibiashara | Sh. 500,000/= kwa tamasha |
| 10. | Matangazo madogo | Sh. 30,000/= kwa tangazo |
| 11. | Kupiga muziki | Sh. 20,000/= kwa siku |
| 12. | Muziki wa Taarabu | Sh. 20,000/= kwa siku |
| 13. | Maonesho ya sinema na video | Sh. 20,000/= kwa siku |
| 14. | Matamasha yasiyo ya kibiashara | Sh. 50,000/= kwa tamasha |
| 15. | Kupiga picha za video | Sh. 20,000/= kwa kila tukio |
| 16. | Mchezo wa fete/Bahatinasibu | Sh. 30,000/= kwa Mwezi |
| 17. | Kupiga muziki Nyumbani | Sh. 20,000/= kwa siku |

RASIMU

## JEDWALI LA TATU

*(Imetengezwa Chini ya kifungu cha 16)*

## HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ………………………nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya.......................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi …………….Mwaka……………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha….…cha Sheria Ndogo ya (Ada za Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ya Mwaka 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya Mwezi…………………..Mwaka …………………………….

*Jina…………………………………..…Saini……………………………………..*

**MBELE YA** :
Jina: ………………………….…………Cheo: …………………………….……

Saini: ……………………………………………
Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa uliofanyika Tarehe ………..mwezi …………… Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikibandikwambele ya:-

...…………………..
**ROBERT MASUNYA**
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Iringa*

…………………………
**STEPHEN MHAPA**
*Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Iringa*

NAKUBALI.................................

**MOHAMED MCHENGERWA (MB)**
***Waziri wa Nchi OR- TAMISEMI***
**TAREHE…………...**
**Dodoma**



RASIMU